

Mambo 7 unayohitaji kufahamu kuhusu chanjo za COVID-19



Jambo #1 Chanjo za COVID-19 hazikuambukizi COVID-19.

Chanjo za COVID-19 hazina sehemu yoyote ya virusi, kwa hivyo haziwezi kukusababishia kupata COVID-19. Chanjo za COVID-19 zinakuinga kutokana na virusi. Unaweza kupata athari baada ya kupata chanjo, kama vile kidonda kwenye mkono au homa. Hizi ni athari za kawaida na watu wengi huzipata.



Jambo #2 Chanjo za COVID-19 ni salama, ingawa zilitengenezwa kwa haraka.

Hakuna hatua zilizorukwa wakati wa kutengeneza chanjo za COVID-19. Wanasayansi ulimwenguni kote wamefanyia utafiti teknolojia hii kwa zaidi ya mwongo mmoja. Hii ndiyo sababu iliwezekana kutoa chanjo salama na yenye ufanisi kwa haraka sana.



Jambo #3 Chanjo za COVID-19 zinaweza kukuinga dhidi ya aina zaidi ya moja ya virusi.

Virusi hubadilika, au hupata mabadiliko kidogo, baada ya muda. Data inaonyesha chanjo za COVID-19 zina ufanisi dhidi ya aina ambazo tumeona hadi sasa za virusi vinavyosababisha COVID-19.



Jambo #4 Chanjo za COVID-19 hazibadilishi DNA yako.

Chanjo za COVID-19 ni chanjo za mRNA na haziingiliani na DNA yako kwa njia yoyote. Zinasababisha mwitikio wa kinga ambao huunda kingamwili ili kukuinga dhidi ya kuambukizwa na COVID-19.



Jambo #5 Chanjo za COVID-19 hazijahusishwa na utasa au kuharibika kwa mimba.

COVID-19 haijasababisha utasa kwa wanawake ambao wamepata virusi, kwa hivyo hakuna sababu ya kufikiria chanjo yake inaweza kusababisha. Kulikuwa na baadhi ya maelezo yaliyoenezwa mtandaoni ambayo yalikuwa **si ukweli**; yaliyodai kuwa protini iliyo kwenye chanjo inashambulia protini kwenye kondo la nyuma. **Hii sio kweli**. Idadi ndogo ya asidi za amino katika protini zote mbili haingeweza kusababisha athari hiyo. Chanjo za COVID-19 hazijafanyiwa majaribio kwa wanawake wajawazito, lakini wanawake wajawazito hupata chanjo za magonjwa mengine wakati wa ujauzito. Wanawake wajawazito wana hatari kubwa ya kupata maradhi makali kutokana na COVID-19 na kuna uwezekano unaweza kumwambukiza mtoto wako COVID-19 baada ya kuzaliwa. Zungumza na daktari wako ili uone ikiwa unapaswa kupata chanjo.



Jambo #6 Chanjo za COVID-19 hazijumuishi chipu ndogo au vifaa vya ufuatiliaji.

Habari potofu kwamba chanjo za COVID-19 zinajumuisha chipu ndogo au vifaa vya ufuatiliaji **imethibitishwa kuwa ya uwongo**. Tunajua haswa kile kimejumuishwa katika kila chanjo. Orodha ya viungo katika kila chanjo inaweza kupatikana [mtandaoni](#).



Jambo #7 Watu wenye magonjwa au matatizo sugu wanapaswa kupata chanjo mara tu zamu yako ya kupata chanjo inapofika.

Ikiwa una ugonjwa sugu, kama vile ugonjwa wa sukari, uko katika hatari kubwa ya kupata maradhi makali kutokana na COVID-19. Chanjo za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi kwa watu walio na magonjwa au matatizo sugu.